#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 11

Julai - Septemba 2023



# 640 KUNUFAIKA 'Samia Scholarship' 2023/2024

## TZS 6.7 bilioni zatengwa

Na Mwandishi wetu
Dar es salaam

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Prof. Adolf Mkenda amezindua awamu ya pili ya Ufadhili wa 'Samia Scholarship' kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika tahasusi za sayansi waliohitimu kidato cha sita mwaka huu (2023) katika mitihani iliyoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) na kueleza kuwa serikali inalenga kuongeza wataalamu na kuimarisha zaidi eneo la fani za Sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati (STEM).

Prof. Mkenda alifanya uzinduzi huo Julai 27, 2023 katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS) kilichopo jijini Dar es salaam ambapo pia alitoa tathmini ya maendeleo ya wanafunzi walionufaika na 'Samia Scholarship' awamu ya kwanza iliyoanza 2022/2023 na kubainisha kwamba jumla ya wanafunzi 636 walidahiliwa na kusajiliwa katika taasisi 18 za Elimu ya Juu nchini.

Kama ilivyokuwa mwaka jana, wanafunzi hao wapya 640 watakaonufaika na ufadhili wa Samia Scholarship mwaka 2023/2024 kwa kugharimiwa kwa asilimia 100 fedha za chakula na malazi, ada ya mafunzo, mahitaji maalumu ya vitivo, gharama za mafunzo kwa vitendo, utafiti, Bima ya Afya na vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

"Ufadhili huo ni kwa masomo ya Shahada ya Kwanza kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu zaidi katika Mitihani ya Kidato cha Sita mwaka 2023 inayoendeshwa na kusimamiwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) katika tahasusi za Sayansi na kuchaguliwa kujiunga na Programu za Sayansi Teknolojia, Elimu Tiba na Hesabu katika Vyuo vikuu nchini", alisema Prof. Mkenda.

Aidha, amefafanua kwamba, majina ya wanafunzi 640 wenye ufaulu wa juu zaidi katika tahasusi za PCB, PCM, PGM, CBG, CBA, PMC na CBN yatatangazwa katika tovuti ya Wizara ya Elimu; www.moe.go.tz na ya HESLB; www.heslb.go.tz kabla ya kufunguliwa kwa dirisha la maombi ya ufadhili kwa mwaka huu.

Maombi ya ufadhili wa Samia Scholarship kwa wanafunzi wa Kitanzania watakaodahiliwa kusoma katika vyuo vya elimu ya juu ndani ya nchi, yatawasilishwa HESLB kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa https://olas.heslb.go.tz kwa muda wa majuma mawili kuanzia Jumatatu, Septemba 25, 2023.

Sambamba na hilo imebainishwa kwamba kwa mwaka wa masomo 2023/2024 Wizara imetenga zaidi ya Shilingi Bilioni 6 kuwezesha utekelezaji wa mpango wa ufadhili na kubainisha kuwa lengo la ufadhili huu ni kuongeza idadi ya wanasayansi nchini ambao watachangia na kuongeza chachu katika maendeleo ya viwanda nchini.
"… mwaka wa masomo 2022/2023 shilingi bilioni tatu zilitengwa na kunufaisha wanafunzi 636 ambapo Kati ya wanafunzi hao, wa kike walikuwa 261 (41%) na wa kiume 375 (59%)", Alisema Prof. Mkenda.

Serikali imetenga TZS 6.7 bilioni kwa mwaka wa masomo 2023/2024 zitakazowanufaisha jumla ya wanafunzi 1,276; wakiwemo wa mwaka wa kwanza (640) na wa mwaka wa pili (636).

## JAMBO LETU



Jacqueline Msuya
*Mhariri*

## Tunawakaribisha wanufaika wapya wa mikopo 2023/2024

Mwaka mpya wa masomo 2023/2024 kwa vyuo vya elimu ya juu hapa nchini unakaribia kufunguliwa mwishoni mwa mwezi Oktoba mwaka huu, ukiashiria wanafunzi wapya nao wanajiunga na elimu ya ngazi hiyo ya juu wakitoka ama Kidato cha Sita ama ngazi ya Stashahada.

Upya kwa tafsiri ya haraka ni hali ambayo haikuwepo awali au zamani, kwamba si kongwe. Hali ya upya inaweza kufananishwa na wanafunzi wapya katika vyuo vya elimu ya juu ikimaanisha hawakuwepo ama katika ngazi hiyo ya elimu au hawakuwepo katika chuo husika au ndio wamepata mikopo kwa mara ya kwanza japo walikuwa tayari chuoni. Upya unaandamana na kutokuwa na uzoefu wa eneo au taratibu mpya. Sasa kwa upande wa wanafunzi wapya wa mwaka wa kwanza, kutokana na kwamba wengi wao ni wageni wa ngazi ya elimu ya juu na mazingira ya taasisi za ngazi hiyo, wanayo mengi wanayotakiwa kujifunza ili kwenda sawia na mazingira ya elimu ya juu.

HESLB kwa kutambua hilo, inawahimiza wanafunzi wenye sifa watakaopangiwa mikopo kuwa na kiu ya kujifunza taratibu za taasisi walikodahiliwa na zaidi kuitambua ofisi inayoshughulikia mikopo ya wanafunzi iliyopo katika kila chuo.

Ni muhimu kwa wanufaika wapya wa mikopo kutimiza wajibu huu wa msingi mara wafikapo vyuoni kutokana na jukumu la ofisi inayosimamia mikopo kuwa kiunganishi kati ya HESLB, mwanafunzi mnufaika na chuo alipodahiliwa.

Kwa kawaida vyuo takriban vyote vya elimu ya juu huweka ratiba ya wiki moja au zaidi ya kuwa na mafunzo elekezi ya taratibu za chuo (orientation week) na huduma za wadau muhimu kwa ustawi wa wanafunzi. HESLB inavishukuru vyuo vya elimu ya juu kwa kuizingatia na kuiweka katika ratiba kila mwaka wa masomo unapoanza ili kuwaelimisha wanafunzi wapya juu ya wajibu wao na kusisitiza matumizi sahihi ya fedha za mikopo.

HESLB hutumia fursa hiyo ya 'orientation week' kuvifikia vyuo kwa lengo la kuwapatia taarifa za moja kwa moja wanafunzi wapya waliopangiwa mikopo kuhusu wajibu wao katika kipindi chote wanapokuwa masomoni. Katika muda huo pia HESLB hupata nafasi ya kupokea maoni kutoka kwa wanufaika.

Licha ya kwamba mnyororo wa utoaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kuanzia kuomba hadi malipo ni kwa njia ya mfumo ambapo mwombaji hutengeneza akaunti yake ya kudumu (SIPA) wakati wa kuomba mkopo, akaunti anakopata taarifa zake za mkopo; Jambo letu leo ni kuwasisitiza wanafunzi wapya kuhakikisha wanatembelea ofisi ya kusimamia mikopo kwa 'Loan Officer' ili kuhakiki taarifa za msingi kabla ya kupokea mkopo zikiwemo namba ya simu na akaunti ya benki. Ni katika ofisi ya mikopo ambapo uratibu hufanyika iwapo kuna masahihisho au nyongeza ya taarifa mpya za mwanafunzi kuhusu mkopo wake.

Kila la heri kwa wanufaika wapya wa mikopo na karibuni sana elimu ya juu.

## NDANI...




03
**LILIAN:**
HESLB msichoke, wanufaika mikopo warejeshe



06
HESLB na TPC zasaini makubaliano kimkakati



08
**Fatma:**
Waombaji mikopo zingatieni Taratibu mjaze fomu kwa usahihi

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**
Omega Ngole

**Mhariri**
Jacqueline Msuya

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi

**Designer**
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Jengo la PSSSF,
Barabara ya Makole,
eneo la Uhindini
S.L.P 984, Dodoma

**Simu:**
+255 758 067577
+255 739 067577

**Barua pepe:**
dodoma@heslb.go.tz

**Tovuti:**
www.heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



# TZS 0.73 Trilioni kunufaisha Wanafunzi 220,376 mwaka 2023/2024

Ni toleo la 11 la Jarida hili la Mtandao mahsusi kwa ajili ya kukupatia kwa muhtasari yaliyojiri HESLB ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku na pia matukio muhimu ya kitaifa yaliyofanyika katika sekta ya elimu hususan elimu ya juu katika robo ya kwanza ya mwaka 2023/2024.

Tukio kubwa zaidi kwa upande wa HESLB katika kipindi hiki ni kuanza kwa msimu mpya wa maombi ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu ikiwa pia ni maandalizi ya kuanza kwa mwaka mpya wa masomo 2023/2024.

Msimu mpya huanza kwa kutangazwa kwa mwongozo wa utoaji mikopo kwa mwaka husika. Mwongozo huo hutaja sifa, masharti na utaratibu wa kuomba mikopo kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa stahiki. Uzinduzi wa msimu mpya ulifanyika Julai 13, 2023 katika ofisi za HESLB jijini Dar es salaam na kuongozwa na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Omari Kipanga.

HESLB na Serikali kwa ujumla inahakikisha utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unafanyika kwa ufanisi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA iliyoboreshwa ukiwemo mfumo mpya wa malipo ya wanafunzi kidigitali utakaoanza kutumika mwaka mpya wa masomo 2023/2024 ambapo mwanafunzi mnufaika aliyekwishasajiliwa kwenye mfumo, atapokea ujumbe wa kujulishwa kiasi cha mkopo na kipengele husika kisha atakiri kupokea kupitia simu yake na baada ya hapo ataweza kutoa fedha zake kwa ajili ya matumizi.

Mwaka huu 2023/2024 bila shaka utakuwa wa mafanikio zaidi kuanzia uchambuzi na upangaji mikopo hadi urejeshaji mikopo kwa kuzingatia miongozo ya utendaji, uwajibikaji na utoaji huduma kwa wateja kwa tija na usawa.

Kipekee nitoe shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa utashi wake wa kuidhinisha TZS 731 bilioni kugharimia masomo ya wanafunzi wa elimu ya juu kwa mwaka huu 2023/2024 ambazo zitawanufaisha wanafunzi takriban 220,376 wakiwemo 75,000 wa mwaka wa kwanza. Hii inamaanisha wanafunzi wa Tanzania wana uhakika wa kusoma katika ngazi zote za elimu kwa ufadhili wa Serikali.

Shukrani pia kwa usimamizi wa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ikiongozwa na Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda na Bodi ya Wakurugenzi wa HESLB ikiongozwa na Profesa Hamisi Dihenga; chini ya uongozi wao, HESLB imekuwa imara zaidi kiutendaji.

Tunazishukuru na kupongeza utayari wa Menejimenti za Taasisi za Elimu ya Juu takriban 100 ambazo zinatoa mafunzo kwa wanafunzi wanufaika wa mikopo kwa kuhakikisha muda wote zinaziwezesha ofisi za kusimamia mikopo ya wanafunzi na hivyo kuwa na ushirikiano mzuri baina ya HESLB, chuo na mwanafunzi.

Ongezeko la fedha za mikopo linaashiria ongezeko la wanafunzi; Menejimenti ya HESLB imejipanga kuendelea kusimamia utoaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu kulingana na ustahiki wa wanafunzi wahitaji wanaolengwa kunufaika kwa kugharimiwa masomo yao kwa mwaka 2023/2024 na vilevile kuimarisha mikakati ya makusanyo ya mikopo kutoka kwa wanufaika ambao mikopo yao imeiva na wanarejesha ili kuchangia wastani wa 30% kwenye mfuko wa mikopo ya wanafunzi.

> *HESLB na Serikali kwa ujumla inahakikisha utoaji na urejeshaji wa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu unafanyika kwa ufanisi kwa kutumia mifumo ya TEHAMA iliyoboreshwa ukiwemo mfumo mpya wa malipo ya wanafunzi kidigitali utakaoanza kutumika mwaka mpya wa masomo 2023/2024*

# Waziri Kipanga aonesha moshi mweupe kwa wanafunzi ngazi ya Stashahada



TUMEFUNGUA DIRISHA LA "SAMIA SKOLASHIPU"

SEPTEMBA, 25 2023 - OKTOBA, 15 2023

Na Mwandishi Wetu
Dodoma

Serikali imejipanga kuanza kutoa mikopo katika ngazi ya Stashahada (Diploma) kuanzia mwaka wa masomo 2023/2024 ili kuongeza idadi ya wataalamu wa kada za fani za kipaumbele katika ngazi hiyo.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mheshimiwa Omary Kipanga alibainisha hayo Julai 13, 2023 jijini Dar es salaam wakati akizindua 'Mwongozo wa Uombaji Mikopo ya Elimu ya Juu kwa Mwaka wa Masomo 2023-2024'.

Licha ya kutaja neema hiyo kwa wanafunzi wanaotarajia kujiunga na vyuo vya kati mwaka huu, Mhe. Kipanga aliwashihi wanafunzi hao kuwa na subira na kwamba mwongozo kuhusu utoaji mikopo kwa ngazi hiyo unaandaliwa na kisha kutangazwa ili kuwawezesha wanafunzi wenye sifa kuomba.

Kuhusu mikopo ya elimu ya juu, Mhe. Kipanga alisema kuwa Serikali imetenga TZS 731 bilioni zitakazowanufaisha jumla ya wanafunzi 220,376 katika mwaka wa masomo 2023/2024.

Akizungumza katika hafla hiyo iliyofanyika katika ofisi za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) zilizopo eneo la TAZARA jijini Dar es salaam, Naibu Waziri Kipanga alisema kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kutoka TZS 654 bilioni zilizotolewa na Serikali katika mwaka uliopita 2022/2023.

"Dhamira ya Serikali kuwawezesha vijana wa kitanzania kupata elimu ya juu inaonekana kwa vitendo," alisema Naibu Waziri Kipanga na kuwasihi wanafunzi waombaji mikopo kuusoma na kufuata maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo huo wa Uombaji Mikopo unaopatikana katika tovuti za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (www.moe.go.tz) na tovuti ya HESLB (www.heslb.go.tz).

Aidha, kwa upande wa mabadiliko ya utaratibu wa kuomba na kuwasilisha maombi HESLB, Mhe. Kipanga alisema kuwa kuanzia mwaka huu, waombaji mkopo hawalazimiki kutuma nakala ngumu (hard copies) na kuongeza kuwa maombi yote yanawasilishwa na kuchambuliwa kwa mfumo na mwombaji kupata mrejesho kupitia akaunti aliyofungua kuombea mkopo (Student's Individual Permanent Account) maarufu kama SIPA.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya HESLB Prof. Hamisi Dihenga alizungumza katika hafla hiyo na kufafanua kwamba baada ya uzinduzi wa mwongozo, HESLB itaendesha programu za elimu kwa umma kupitia redio, runinga, mitandao ya kijamii na mikutano ya moja kwa moja.

Maafisa wa HESLB wameendelea kutoa elimu ya uombaji mikopo kwa wanafunzi wa Kidato cha sita kati ya mwezi Julai na Septemba, 2023 katika shule za sekondari 35 zilizopo mikoa ya Dodoma, Dar es salaam, Arusha, Mwanza, Mbeya na Mtwara na kugawa mabango na vipeperushi vyenye taarifa za utaratibu na nyaraka muhimu katika uombaji mikopo ambavyo pia vilifikishwa Makao Makuu ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) kwa lengo la kugawiwa kwenye kambi zote 20 ambako wanafunzi waliohitimu Kidato cha Sita mwaka huu walikuwa wanaendelea na mafunzo kwa mujibu wa Sheria.

Katika utaratibu huo endelevu wa utoaji elimu kwa umma, HESLB pia inashiriki katika vipindi na kutoa matangazo kupitia vyombo vya habari na mitandao ya jamii ili kufikisha ujumbe kwa walengwa wengi zaidi.

# LILIAN:

## HESLB msichoke, wanufaika mikopo warejeshe

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

Mwalimu Lilian Sefue wa Shule ya Msingi Umoja wa Mataifa iliyopo Halmashauri ya Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam, ameipongeza HESLB kwa kazi nzuri inayofanya ya kusaka wadaiwa wa mikopo ya elimu ya juu na kuiomba isichoke kufanya kazi hiyo, kwa kuwa bila mikopo kurejeshwa vijana wengi wahitaji wanakosa fursa ya kusoma vyuo vikuu.

Mwalimu Lilian amejitokeza na kulipa mkopo wake wote uliokuwa umebaki, kiasi cha Shilingi milioni sita laki nne na elfu sitini na nne (6,464,000), baada ya kuona wazazi wengi wanakuwa na wasiwasi mkubwa wa jinsi ya kumudu gharama za chuo kikuu, na hivyo akaona umuhimu wa kurejesha ili kuwawezesha watanzania wengine wenye uhitaji nao wapate fursa ya kusoma elimu ya juu.

Mwalimu Lilian ambaye alipata Shahada ya Sanaa ya Ualimu na Maendeleo ya Jamii katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania (IAE), na kuhitimu mwaka 2018, amejikita katika kufundisha Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) ambapo anafundisha madarasa ya awali yaani darasa la kwanza na la pili.

"…Kazi yangu kubwa ni kuwajengea msingi mzuri watoto hawa wadogo ambao natamani wafike hatua kama yangu au zaidi hapo mbeleni. Mimi nilikopeshwa na serikali nikatimiza ndoto zangu, natamani hawa watoto pia wapate fursa hiyo, na hicho hasa ndicho kilinisukuma nikaona nirejeshe mkopo wangu wote nikiamini utasaidia kutimiza ndoto za mtanzania mwingine…", anaelezea Mwalimu Lilian.

Kwa upande mwingine, Mwalimu Lilian ameishauri HESLB isichoke na iongoze kasi ya kuwasaka wadaiwa wa mikopo ya elimu ya juu, kwa kutoa elimu zaidi kwa umma na kushirikiana na waajiri katika kuwabaini ili mikopo hiyo ilipwe kwa wakati.

"Najua suala la kurejesha mkopo wowote ule huwa ni gumu sana, ila naishauri HESLB isichoke kusaka wadaiwa, na iongeze juhudi zaidi katika kuwasaka wanufaika wa mikopo ambao hawajaanza kabisa kurejesha mikopo yao, kwa kutoa elimu na kushirikiana na waajiri, ili wadaiwa wengi walipe mikopo yao, iwasaidie watanzania wengine wanaojiunga na vyuo vikuu …", anasisitiza Mwalimu Lilian.

Mwalimu Lilian anatoa wito pia kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu ambao wana kipato na bado hawajaanza kurejesha mikopo waliyopewa na serikali, wawe wazalendo, wajitokeze na kurejesha mikopo yao ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuendelea kusomesha watanzania wengi ngazi ya elimu ya juu.


Wahenga wanasema, "Atafutaye hachoki na akichoka keshapata", HESLB tunaendelea kukusanya mikopo bila kuchoka na kubuni mbinu mpya kila mara ili kuhakikisha mikopo iliyoiva inarejshwa kwa wakati.




**Mwalimu Lilian amejitokeza na kulipa mkopo wake wote uliokuwa umebaki, kiasi cha Shilingi milioni sita laki nne na elfu sitini na nne (6,464,000), baada ya kuona wazazi wengi wanakuwa na wasiwasi mkubwa wa jinsi ya kumudu gharama za chuo kikuu...**



**Julai 11,2023:** *Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya HESLB ikiwa katika Ofisi za Mpango wa Serikali nchini Afrika Kusini unaotoa usaidizi wa kifedha kwa Wanafunzi wanaosoma elimu ya juu wasio na uwezo wa kujigharimia masomo (National Student Financial Aid Scheme - NSFAS) kwa ziara ya kubadilishana uzoefu iliyofanyika Julai 11-14,2023, jijini Cape Town. Kutoka kushoto ni Mkurugenzi Msaidizi wa TEHAMA, Bahati Singa, Meneja Mawasiliano, Veneranda Malima, Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala na Rasilimali Watu, Gibson Mayani, Mkurugenzi Msaidizi wa Urejeshwaji Mikopo, Phidelis Joseph pamoja na Mkurugenzi Msaidizi wa Ununuzi na Ugavi, Sadiki Sangawe.*



**Julai 18, 2023:** *Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto) akisalimiana na Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru (wa pili kulia) katika kilele cha Maonesho ya 18 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia yaliyofanyika Julai 18-22, 2023 katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es salaam.*




**Agosti 17,2023:** *Maafisa kutoka HESLB (katikati waliovaa mashati ya bluu) wakiwa katika picha ya pamoja na wanafunzi wa kidato cha tano na sita wa shule ya Sekondari Misungwi mkoani Mwanza, mara baada ya kumaliza kipindi cha utoaji elimu ya masuala ya uombaji mikopo ya elimu ya juu.*



**Agosti 2, 2023:** *Afisa Habari na Uhusiano-HESLB, Abdullah Khamis, akihudumia wateja waliofika kupata huduma katika banda la HESLB katika Maonesho ya nne ya Wiki ya Elimu ya juu Zanzibar yaliyofanyika Julai 30 - Agosti 5, 2023 katika Viwanja vya Maisara, Zanzibar.*



**Agosti 1, 2023:** *Ujumbe wa HESLB, pamoja na wenyeji wakifuatilia mada iliyokuwa ikiwasilishwa na Mkurugenzi Msaidizi wa Habari, Elimu na Mawasiliano, Omega Ngole (hayupo pichani). HESLB ilikutana na Shirika la Wanafunzi wa Korea (Korea Student Aid Foundation-KOSAF) Julai 30 – Agosti 3, 2023 katika mji wa Daegu nchini Korea Kusini.*




# Wahi Chap!

## Taarifa sahihi toka mitandao yetu ya kijamii

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

Soma taarifa kupitia kurasa za mitandao ya kijamii za HESLB kwa jina la HESLB Tanzania kisha sambaza tabasamu na furaha kwa wengine ili kujenga future yako!

Kwa Lugha nyepesi ni kwamba kurasa za mitandao ya kijamii za HESLB (Facebook na Instagram) sasa zinatambulika rasmi kwa wadau na wateja baada ya kupata Uthibitisho yaani tiki ya bluu (Blue tick checkmark) kwa uratibu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA).

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano HESLB, Omega Ngole amesema 'Blue Tick' kwa HESLB ina umuhimu mkubwa kutokana na huduma za taasisi hiyo za upangaji, utoaji na urejeshaji mikopo ya elimu ya juu kugusa maslahi ya Watanzania wengi.

"Tunawasihi wadau na wateja wetu waendelee kufuatilia kurasa zetu kwenye mitandao hiyo kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali za uhakika kutoka HESLB", amesema Ngole.

Ngole ameongeza kuwa Taasisi za umma zimekuwa mstari wa mbele kuongeza idadi ya wasomaji na wafuasi wa taarifa zake kupitia mitandao ya kijamii ili kujenga ushawishi na kutangaza huduma za umma kwa jamii ili kuepusha upotoshaji wa maudhui mitandaoni unaoweza kuibua taharuki katika jami.

Blue tick katika kurasa za mitandao za HESLB zinamaanisha kurasa hizo ni rasmi kwa ajili ya taarifa na habari zinazotolewa na HESLB kwenda kwa wadau na kwamba zimethibitishwa kwa mujibu wa taratibu za usajili wa mitandao ya kijamii Tanzania.

Kuhusu ukurasa wa X (zamani Twitter) wa HESLB ambao bado haujathibitishwa, Ngole amewatoa hofu wadau na wateja kuhusu uhakika wa taarifa zinazotumwa kupitia ukurasa huo kwa sasa kwamba zinaaminika kwa kuwa taratibu za awali za usajili wa ukurasa huo zimekamilika na muda wowote kuanzia sasa, pia utapatiwa alama ya tiki ya bluu.

Kurasa za mitandao ya kijamii za HESLB Tanzania (Facebook, Instagram na Twitter) ilianza kutumiwa na HESLB miaka nane (8) iliyopita na mwezi Novemba mwaka 2021, HESLB ilianza utaratibu wa kuthibitisha rasmi kurasa zake za mitandao hiyo ya kijamii ambapo mwezi Aprili, 2023 ukurasa ya Facebook ulithibitishwa na baadae mwezi Julai mwaka huu ukurasa wa Instagram pia ulipata Blue tick.




*Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB Abdul-Razaq Badru (kushoto) akipeana mkono na aliyekuwa Postamasta Mkuu (TPC), Macrice Mbodo baada ya kusaini makubaliano ya kimkakati.*

# HESLB na TPC zasaini makubaliano kimkakati

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

> **Mpaka sasa tuna 'internet cafés' zaidi ya 36 na madirisha zaidi ya 100, lengo ni kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza malengo yake ya kila mwanachuo kupata mkopo,**

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imesaini makubaliano ya kimkakati na Shirika la Posta Tanzania (TPC), ili kurahisisha huduma ya uombaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji wanaotarajia kujiunga na vyuo vya elimu ya juu ili kuwawezesha waombaji mikopo kupata unafuu na usaidizi makini katika kipindi ambapo dirisha la uombaji mikopo lipo wazi.

Katika hafla ya utiaji saini iliyofanyika Agosti 24, 2023 katika Ofisi ya Makao Makuu ya TPC jijini Dar es salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru alisema kwa sasa taasisi hizo mbili za umma zinakoleza mashirikiano ya huduma kwa kuwa zilishaanza kushirikiana muda mrefu katika kuwasaidia wanafunzi kufikia ndoto zao.

"Dirisha la maombi lipo wazi tangu lifunguliwe Julai 15, 2023 na litafungwa Oktoba 15, 2023, hivyo ni fursa kwa waombaji wote kutembelea vituo vya huduma ya 'internet' vya TPC ili kupata msaada wa kufanya maombi kupitia mtandao," alisisitiza Badru.

Kwa upande wa TPC, aliyekuwa Postamasta Mkuu, Macrice Mbodo wakati wa utiaji saini alisema kuwa makubaliano hayo yatawawezesha waombaji wa mikopo kuomba mikopo kwa usahihi kutokana na usaidizi makini wanaoupata kutoka katika vituo vya TPC vyenye watumishi wenye weledi na kuwatoa wasiwasi kwamba huduma zote zinapatikana sehemu moja kupitia Huduma Pamoja inayowaunganisha wadau wengine kama RITA (Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini).

"Mpaka sasa tuna 'internet cafés' zaidi ya 36 na madirisha zaidi ya 100, lengo ni kumsaidia Mheshimiwa Rais kutimiza malengo yake ya kila mwanachuo kupata mkopo,". Sambamba na hilo tuna vifaa vya kutosha kuwezesha waombaji wa mikopo kufikia malengo waliyojiwekea ya kusoma elimu ya juu kwa kupata mikopo ambayo Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliahidi kutekeleza kwa kiwango kikubwa", alisema Mbodo.

HESLB imefanya mabadiliko katika mifumo yake ili kuwezesha waombaji mikopo kujihudumia wenyewe kwa kujaza taarifa zao na viambatisho husika kwenye mfumo na hawalazimiki tena kutuma nakala ngumu ya maombi HESLB kama ilivyokuwa miaka ya nyuma.

Makubaliano ya kimkakati baina ya HESLB na TPC yaliyoshuhudiwa na watumishi wa taasisi zote mbili na waandishi wa habari, yanatarajiwa kuongeza ufanisi na kurahisisha mchakato wa kuomba mikopo kwa wanafunzi kwa kuwa na uhakika wa kufikia huduma ya 'internet cafes' za uhakika za TPC zilizoenea nchi nzima Tanzania Bara na Zanzibar.



# FATMA:

## Waombaji mikopo zingatieni Taratibu mjaze fomu kwa usahihi

Na Mwandishi Wetu
Dar es Salaam

> **...Nilipopata fursa ya kuomba mkopo nilihakikisha najaza kwa umakini mkubwa maana niliogopa nikikosa mkopo wazazi wasingeweza kunisomesha chuo kikuu...**

Fatma Mbaruku Abbas, binti mwenye umri wa miaka ishirini na nne (24) na mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al-Sumait maarufu SUMAIT kilichopo Chukwani, Zanzibar, amewashauri waombaji mikopo wa elimu ya juu kuzingatia taratibu zinazotolewa na HESLB ili kujaza fomu za maombi ya mkopo kwa usahihi na kuweza kukopeshwa ili watimize ndoto zao.

Fatma ni mwanafunzi wa mwaka wa kwanza 2022/2023 wa Shahada ya Sanaa katika Ushauri Nasaha na Saikolojia (Bachelor of Arts in Counselling and Psychology - BCP) ambaye anasema isingekuwa mkopo wa elimu ya juu, ndoto zake za kuendelea na chuo kikuu zisingetimia.

Akiongea na HESLB Yako, Fatma amewasihi waombaji mikopo hasa wanaotoka kwenye familia ambazo wazazi hawawezi kumudu gharama za kusomesha watoto wao vyuo vikuu, kuhakikisha wanasoma mwongozo wa utoaji mikopo na kujaza fomu za maombi kwa kufuata taratibu wanazoelekezwa na HESLB.

"...Tumezaliwa watoto nane (8) na mimi ni wa kwanza kuzaliwa. Baba yangu ni mfanyabiashara mdogo anayeuza vitu vya urembo kama hereni, bangili na mikufu. Mama yangu anafanya shughuli za nyumbani na kutulea. Nilipopata fursa ya kuomba mkopo nilihakikisha najaza kwa umakini mkubwa maana niliogopa nikikosa mkopo wazazi wasingeweza kunisomesha chuo kikuu...", anaelezea Fatma.

Aidha, Fatma anaishukuru serikali kwa kumkopesha na kuweza kujiunga na chuo kikuu kusoma Shahada ya Sanaa katika Ushauri Nasaha na Saikolojia ambayo anaamini kwa dunia ya sasa watu wengi wana changamoto za maisha ambazo wengine hufikia hatua ya kukatisha maisha yao kwa sababu ya kukosa ushauri.

"...Niliamua kusoma shahada hii ili niweze kuisaidia jamii inayonizunguka, kwa kuwashauri watu wasifikie kwenye maamuzi mabaya wanapokumbana na changamoto za maisha bali watafute namna nzuri ya kukabiliana nazo...", anasema Fatma.

Fatma anaishukuru pia HESLB kwa kumuongezea kiasi cha ada kutoka shilingi laki mbili na mia tano (200,500) alichopangiwa awali hadi shilingi milioni moja na laki mbili (1,200,000) baada ya kuomba nyongeza na anaamini ongezeko hilo limepunguza mzigo mkubwa kwa wazazi wake kutafuta fedha ya kuongezea ili kumlipia ada yote.

Fatma ni miongoni mwa wanafunzi wahitaji wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu tangu mwaka 1995, ili kuwawezesha kufikia malengo yao ya kitaaluma na hatimaye kutumia fani zao kwa manufaa ya jamii inayowazunguka na Taifa kwa ujumla.

HESLB
BODI YA MIKOPO
TUNAWEKEZA KWA KIZAZI CHA BAADAE



# SAMIA SCHOLARSHIP 2023/2024

## SIFA ZA KUPATA UFADHILI

- Awe Mtanzania;
- Awe na ufaulu wa juu kwenye mtihani wa taifa ya kidato cha sita mwaka 2023 iliyoendeshwa na NECTA katika tahasusi za sayansi;
- Awe amepata udahili katika Chuo cha Elimu ya Juu hapa nchini kinachotambuliwa na Serikali katika programu za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati au Tiba
- Awe ameomba ufadhili kwa usahihi kwa njia iliyoelekezwa. https://olas.heslb.go.tz

## MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA:

- Ufadhili huu ni wa asilimia mia moja ambao kikomo chake kitazingatia miongozo ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.
- Orodha ya majina ya wanafunzi husika inapatikana kupitia www.moe.go.tz na www.heslb.go.tz

- Ni kwa masomo ya shahada ya kwanza kwa wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika mitihani ya Kidato cha Sita mwaka 2023
- Mitihani iliyoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) katika Tahasusi za Sayansi (PCB, PCM, PGM, CBG, CBA, PMC na CBN).
- Itagharimia kwa asilimia mia moja (100%) masomo ya Elimu ya Juu kwa wanafunzi 640 ambao wamepata udahili katika fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati na Tiba mwaka huu 2023/2024.

HESLB Tanzania HESLB Tanzania HESLB_Tanzania

#Kazilendelee
#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu

## DODOMA

Jengo la PSSSF,
Br. Makole, eneo la Uhindini

S.L.P 984,
Dodoma

+255 758 067577

+255 739 067577

dodoma@heslb.go.tz

## HUDUMA KWA WATEJA

PSSSF Twin Tower
Ghorofa ya chini
Mtaa wa Misheni
S.L.P 76068,
Dar es Salaam
Simu: +255 758 067 577
+255 739 067 577
Email: info@heslb.go.tz

## DAR ES SALAAM

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, Tazara,
Br. Mandela
S.L.P 76068, 15471
Dar Es Salaam
Simu: 0736 665 533
Email: info@heslb.go.tz

## ZANZIBAR

Jengo la Michenzani Mall,
Eneo la Michenzani
Ghorofa ya Tano
S.L.P 900, Zanzibar,
Simu: 0779 321 424
Email: zanzibar@heslb.go.tz

## ARUSHA

NSSF Jengo la Mafao,
Ghorofa ya Kwanza
S.L.P 2712, Arusha
Simu: 027 2520128
0624 100 011
0739 102 016
Email: arusha@heslb.go.tz

## MWANZA

PSSSF Plaza, ghorofa ya pili
Br. Kenyatta
S.L.P 3051, mwanza
Simu: 028 2506008
0759 819 350
0738 153 661
Email: mwanza@heslb.go.tz

## MBEYA

Jengo la CAG, Br. Mbalizi
S.L.P 319, Mbeya
Simu: 0738 131 310
0738 131 311
Email: mbeya@heslb.go.tz

## MTWARA

NHC Raha Leo Complex,
Ghorofa ya pili
S.L.P 969, Mtwara
Simu: 0736 026 668
Email: mtwara@heslb.go.tz